**HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**

**SAYANSI NA TEKNOLOJIA DARASA LA NNE, OKTOBA 2024**

**SEHEMU A: (Maksi 30)**

**1. Chagua herufi ya jibu sahihi na uandike kwenye kisanduku ulichopewa**

**i.** Zakaria alitaka kujua urefu wa chumba. Ni kipi kati ya vifaa vifuatavyo alikitumia?
**(A)** Amita (B) Kipima ujazo (C) Kipima joto (D) Tepu [ ]

**ii.** Wakati mwalimu wa sayansi kutoka shule ya msingi Likon'go akiwafundisha darasa la nne kuhusu kinga ya mwili alieleza kazi ya seli nyeupe za damu mwilini. Ni ipi kati ya zifuatazo ni kazi ya seli nyeupe za damu?
(A) Kujenga mwili (B) Kusafirisha oksijen (C) Kulinda mwili dhidi ya magonjwa
(D) Kuupa mwili nishati [ ]

iii. Viumbe hai wana sifa mbalimbali. Kitendo cha kiumbe hai kutoa taka mwilini kinaitwa ____
(A) Kujongea (B) Kukua (C) Kuzaliana (D) Utoaji takamwili [ ]

iv. Malaria ni ugonjwa wa kuambukiza unaosabaishwa na kimelea kinachoitwa?
(A) Anofelesi jike (B) Plasmodiam (C) Anofelesi dume (D) Mbu kyuleksi [ ]

v. Joto husafiri katika maada yabisi kwa njia ya
(A) Mpitisho (B) Msafara (C) Mnutudisho (D) Kipitisha mwanga [ ]

**2. Oanisha fungu A na fungu B ili kuleta maana kamili**

| NO | FUNGU A | MAJIBU | FUNGU B |
|---|---|---|---|
| i. | 212°F | [ ] | A. Mmeng'enyo wa chakula huuanzia hapa |
| ii. | Skrini | [ ] | B. Hutabiri matokeo ya uchunguzi |
| iii | Matege | [ ] | C. Kizingiti cha mgando cha maji |
| iv | Iliamu | [ ] | D. Ufyonzaji wa chakula |
| v. | Dhanio | [ ] | E. Upungufu wa vitamini C |
| | | [ ] | F. Kizingiti cha myeyuko cha maji |
| | | | G. Huonesha picha na maandishi<br>H. Upungufu wa vitamini D |

**3. Jaza sehemu zilizo wazi kwa kutumia maneno yaliyo kwenye kisanduku**

| Maada | Ripoti | Hewa ya oksijeni | maji | huduma ya kwanza | nishati |
|---|---|---|---|---|---|

**i.** ____________________ ni msaada wa haraka anaopatiwa majeruhi.
**ii.** Maada inayopatikana katika hali zote tatu ni ______________________
**iii.** Kitu chochote chenye uzito na kinachochukua nafasi huitwa ________________________
**iv.** _____________________ hutumika katika mwili kuunguza chakula na kuzalisha nishati
**v.** ___________ huandikwa baada ya uchunguzi wa kisayansi kwa lengo la kutunza taarifa kwa matumizi ya baadae.

**4. Panga upya hatua za kufanya uchunguzi wa kisayansi kuanzia ya kwanza hadi ya mwisho**

**i.** Kukusanya data [ ]
**ii.** Kubuni dhanio [ ]
**iii.** Kubaini tatizo [ ]
**iv.** Hitimisho [ ]
**v.** Kufanya jaribio [ ]

**5. Jaza nafasi zilizo wazi**

i. Vyakula vinavyojenga mwili vinaitwa__________________________
ii. _____________________ ni uwezo wa mwili kupambana dhidi ya magonjwa
iii. Taja aina mbili za majiko yanayochangia ukataji wa miti hovyo
(a) _________________________________________
(b) __________________________________
iv. Kitendo cha kusafirisha taarifa kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine kinaitwa
_________________________

v. Ili chakula kidumu kwa muda mrefu bila kuharibika kinatakiwa kuhifadhiwa kwenye kifaa kinachoitwa

______________________________________